# Vifupisho

| | |
|---|---|
| AAITz | ActionAid International Tanzania |
| CEDAW | Mkataba wa Kuondoa  Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake |
| DV | Ukatili unaofanyika majumbani |
| FGD | Mjadala wa kikundi cha walengwa |
| FGM | Ukeketaji |
| GBV | Ukatili wa kijinsia |
| JUWAKAP | Jumuiya ya Wanawake Kaskazini Pemba |
| JUWAMAKU | Jumuiya ya Wanawake na Maendeleo Kaskazini Unguja |
| MLYWCD | Wizara ya Kazi, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto (jina la zamani) |
| MSYWCD | Wizara ya Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Maendeleo ya Watoto (jina la sasa) |
| NGO | Shirika Lisilokuwa la Kiserikali |
| PF3 | Fomu ya Polisi Na. 3 |
| SADC | Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi Kusini mwa Afrika |
| SOSPA | Sheria ya Makosa ya Kujamiiana |
| SV | Ukatili unaohusisha Ngono |
| TAMWA | Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania |
| TPFNet | Mtandao wa Polisi Wanawake Tanzania |
| UNFPA | Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Idadi ya Watu |
| UNICEF | Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa |
| UNSCR | Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa |
| VAW | Ukatili Dhidi ya Wanawake |
| WHO | Shirika la Afya Duniani |
| ZAFELA | Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar |
| ZLS | Chama cha Wanasheria Zanzibar |
| ZLSC | Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar |

# Dibaji

Kila ifikapo mwezi Novemba duniani kote, wale ambao wamefanya maisha yao kuwa ni kazi ya kupambana na ukatili dhidi ya wanawake, hupumzika kidogo na kufanya maadhimisho ya siku muhimu sana.

Tofauti na siku inayofanana nayo ambayo hujulikana zaidi – yaani Siku ya Wanawake Duniani – Siku ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake Duniani, haijulikani sana. Na hata kisichojulikana zaidi ni simulizi ya wakina dada watatu kutoka Jamhuri ya Dominika, ambao waliutia hamasa Umoja wa Mataifa kutenga siku maalumu ya kuwakumbuka.

Tunapoandaa ripoti hii, siwezi kujizuia kuwafikiria madada hawa wakina Mirabal na vuguvugu lao la kishujaa kupambana na ukatili usioisha unaohusisha ngono na mateso ya kisaikolojia. Ni zaidi ya miaka hamsini iliyopita, madada hawa walipigwa kikatili hadi kufa. Ushujaa waliouonyesha mbele ya ukatili waliokabiliana nao uliamsha wimbi la ghadhabu, ambalo baadaye lilipelekea kuundwa kwa mikataba na sera za kimataifa.

Lakini balaa la ukatili dhidi ya wanawake bado tunalo. Licha ya mikataba ya kimataifa, na wimbi la sheria mpya za kitaifa duniani kote, lakini bado wakosaji wanaendelea kuwaumiza, kuwavunja viungo na kuwaua wanawake bila ya hofu ya kuadhibiwa. Ukatili dhidi ya wanawake na wasichana ni mojawapo ya ukiukwaji wa haki za binadamu ulioenea sana duniani – mmoja kati ya wanawake watatu duniani atakumbana na ukatili wa kijinsia katika maisha yake, mmoja kati ya watano atakabiliwa na kubakwa au jaribio la kubakwa. Ukatili sio tu sababu kubwa inayosababisha kifo na ulemavu, lakini pia ni sababu inayoongoza katika kuleta umasikini na ukosefu wa amani duniani.

Ripoti hii ni simulizi ya makundi ya wanawake kisiwani Zanzibar ambao, kama ilivyo kwa dada zao duniani kote, wanakoseshwa haki zao. Sababu kwa nini inakuwa hivyo, ziko sawa duniani kote na si kwa Zanzibar au Tanzania peke yake. Kukosekana kwa usawa wa kijinsia, mifumo ya utoaji haki ambayo haipewi rasilimali za kutosha, mifumo ya misaada iliyozidiwa nguvu na matatizo, tamaduni potofu, mitazamo, na **"ukuta wa ukimya"** vyote hivyo vimekula njama ya kuwanyima wanawake hawa haki na misaada wanayostahil.

Ijapokuwa mwanzo wa hadithi ya wanawake hawa ni simulizi ambayo si ngeni duniani, sisi hapa ActionAid tuna matumaini kuwa kwa msaada mkubwa tuliokuwa nao, na tunaoendelea kuupata kutoka Serikali ya Zanzibar na Umoja wa Ulaya kupambana na ukatili visiwani Zanzibar, hadithi zao, inshallah zitakuwa na mwisho tofauti na wa furaha zaidi.



Aida Kiangi
Mkurugenzi, Shirika la ActionAid Interactional Tanzania

# Muhtasari Rasmi

*"Nilihofu na niliona aibu kuwasimulia watu wengine, na baadaye nilimwambia yule mwanamme aniache."*
*Mhanga wa Ukatili Dhidi ya Wanawake, Uchunguzi wa AAITz kuhusu Ukatili Dhidi ya Wanawake*

Ukatili Dhidi ya Wanawake ni ukiukwaji wa haki za msingi za binadamu kwa wanawake. Ni aina ya ubaguzi ambao misingi yake inatokana zaidi na tofauti zilizopo za madaraka na miundo isiyo sawa kati ya wanawake na wanaume.[1] Kufuatana na takwimu zilizopatikana kutoka nchi mbali mbali, kati ya asilimia 15 na 76 ya wanawake duniani kote wamelengwa kufanyiwa shambulio la kimwili au/na ukatili unaohusisha ngono katika maisha yao.[2] ActionAid Tanzania (AATZ) inatekeleza mradi unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya katika mikoa ya Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba ambao unalenga kupunguza na kuzuia matukio ya Ukatili Dhidi ya Wanawake. Uchunguzi huu wa awali kuhusu Ukatili Dhidi ya Wanawake huko Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba una madhumuni ya kutoa taarifa kuhusu mradi huu na umechunguza kuenea kwa aina tofauti za Ukatili Dhidi ya Wanawake; vikwazo vya kupata haki, msaada na usalama kwa waathirika wa Ukatili Dhidi ya Wanawake; na mitazamo na hisia zilizopo kuhusu Ukatili Dhidi ya Wanawake katika ngazi ya jamii Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba.

Uchunguzi huu umegundua kwamba kukosa uelewa wa Ukatili Dhidi ya Wanawake kunazidishwa na uhaba wa utafiti, majadiliano ya jamii na utayarishaji sera hususan kwenye mahitaji ya wanawake watu wazima ambao wanafanyiwa ukatili visiwani Zanzibar. Uchunguzi uliofanyika umeelekea kutilia mkazo katika uchambuzi mpana wa ukatili wa kijinsia (ikijumuisha ukatili dhidi ya watoto na wanaume) au ukatili dhidi ya watoto. Kuanzishwa kwa huduma za kisasa/mpya, kama vile kituo kinachotoa huduma nyingi sehemu moja (Mkono kwa Mkono), kilichobuniwa na shirika la Save the Children, wakati kikishughulikia kesi kadhaa za Ukatili Dhidi ya Wanawake kimezidiwa nguvu na wingi wa matukio, na inaeleweka kwamba wajibu wake wa msingi ni kushughulikia mahitaji ya watoto.

Utamaduni wa aibu na ukimya umegubika Ukatili Dhidi ya Wanawake katika jamii za Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba. Hali hii hufanya iwe vigumu sana kujua kiwango cha kuenea kwa Ukatili Dhidi ya Wanawake na pia husababisha tatizo la matukio mengi kutokuripotiwa. Wanawake wengi waliofanyiwa ukatili hawatafuti msaada kutoka polisi wala huduma nyingine za msaada, ikimaanisha kwamba takwimu kutoka katika taasisi rasmi na tafiti zinazotokana na huduma zilizotolewa zinaweza kuonyesha makadirio ya chini sana ya hali halisi ya ukubwa wa tatizo. Ikichangia kulifanya tatizo hili kuwa kubwa zaidi, ni ukweli kwamba habari kuhusu ukatili dhidi ya wanawake watu wazima au aina nyingine za Ukatili Dhidi ya Wanawake hazikusanywi mara kwa mara na taasisi zinazohusika pamoja na watoa huduma visiwani Zanzibar. Takwimu zinapopatikana hazina ulinganifu na mara nyingi hazipangwi kwa kuzingatia jinsia. Uchunguzi huu umejaribu kumulika mapungufu haya na kuvishawishi vyombo vya kusimamia sheria kutilia maanani mahitaji ya wanawake waliofanyiwa ukatili.

[1] Angalia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Kuzidishwa kwa juhudi za kuondoa aina zote za ukatili dhidi ya wanawake: ripoti ya Katibu Mkuu, 4 Agosti 2008, A/63/214 na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Uchunguzi wa kina kuhusu aina zote za ukatili dhidi ya wanawake: ripoti ya Katibu Mkuu, 6 Julai 2006, A/61/122/Add.1.

[2] http://www.endvawnow.org/en/articles/299-fast-facts-statistics-on-violence-against-women-and-girls-.html

# Matokeo Muhimu ya Uchunguzi:

## Kuenea kwa Ukatili Dhidi ya Wanawake

- Asilimia 17.2 ya wanawake walioolewa kisiwani Unguja na asilimia 35.6 Pemba wamesema kwamba wameshawahi kupigwa.
- Majibu ya wana jamii walioshiriki uchunguzi yanaonyesha kwamba ukatili unaohusisha ngono unachukuliwa kuwa ni mbaya zaidi kuliko kupiga au mateso ya kisaikolojia. Asilimia 17.2 ya wanawake walioolewa na kushiriki uchunguzi kisiwa cha Unguja na asilimia 33.3 kutoka Pemba walionyesha kwamba walishawahi kufanyiwa ukatili unaohusisha ngono.
- Sehemu kubwa zaidi ya walioshiriki uchunguzi Kaskazini Unguja walisema kwamba wameshawahi kufanyiwa mateso ya kisaikolojia – asilimia 23.4. Hata hivyo, majibu yanayohusiana na udhibiti katika ndoa yanaonyesha kwamba aina hii ya ukatili inaweza kuwa kubwa zaidi Kaskazini Unguja, kukiwa na sehemu kubwa ya wanawake waliolewa wakionyesha kwamba wamewahi kutukanwa na kuzuiwa kutoka nje.
- Kisiwani Pemba, asilimia 57.8 ya wanawake walioolewa walisema kwamba wamewahi kufanyiwa mateso ya kisaikolojia. Matokeo haya kwa kisiwa cha Pemba yanakubaliana na matokeo ya tafiti zilizopita kwamba kiwango cha kuenea kwa Ukatili Dhidi ya Wanawake kiko juu hasa kisiwani Pemba.
- Zaidi ya ukatili unaotokea baina ya wenza walio pamoja, asilimia 11.3 ya wanawake walioshiriki uchunguzi kisiwani Unguja na asilimia 8.3 Pemba walikubali kwamba "ndiyo" walishawahi kufanyiwa ukatili na mtu ambaye si mwenza.
- Asilimia 8.4 ya wanawake walioshiriki uchunguzi Kaskazini Unguja na asilimia 17.8 ya wanawake walioshiriki Kaskazini Pemba ambao wameshawahi kuwa wajawazito walisema kwamba wameshawahi kupigwa wakati wakiwa wajawazito. Zaidi ya robo tatu ya wanawake waliopigwa wakati wa mimba, waliwataja waume wao wa sasa au waliopita kuwa ndio waliofanya ukatili huo.
- Ndoa za utotoni zilitambulika kuwa ni aina ya ukatili ulioenea sana kote Unguja na Pemba. Asilimia 48 ya wanawake walioshiriki uchunguzi Kaskazini Unguja na asilimia 62 Kaskazini Pemba waliolewa wakiwa na umri kati ya miaka 12 na 18.
- Wasichana, ambao huozwa katika umri mdogo, wanakabiliwa na hatari kubwa za kiafya na wana uwezekano mkubwa wa kupata mimba katika umri mdogo. Mkoani Kaskazini Unguja, asilimia 19.1 ya wanawake walio katika umri ambao wanaweza kupata watoto walijifungua wakiwa na umri kati ya miaka 15 hadi 18; na asilimia 4.3 walijifungua wakiwa na umri kati ya miaka 12 hadi 15. Kisiwani Pemba hii iliongezeka hadi asilimia 15.9 kwa wanawake waliozaa mtoto wao wa kwanza wakiwa na umri wa miaka kati ya 12 na 15, na asilimia 34.1 kati ya miaka 15 na 18.
- Kuachwa na kutelekezwa kwa wanawake na waume zao pia kulisisitizwa kuwa ni suala muhimu Unguja na Pemba, pamoja na ubaguzi dhidi ya wanawake katika masuala yanayohusiana na talaka na mirathi.

*"Baba yangu alimwita mume wangu na kumkaripia, halafu nilirudi nyumbani baadaye."*
*Mhanga wa Ukatili Dhidi ya Wanawake, Uchunguzi wa AAITz kuhusu Ukatili Dhidi ya Wanawake*

## Kuelewa na mitazamo kuhusu Ukatili Dhidi ya Wanawake

- Watu wengi walioshiriki uchunguzi Kaskazini Unguja walipoulizwa wanafikiria ni ukatili wa aina gani dhidi ya wanawake ndio unaotokea mara nyingi zaidi katika jamii yao, walitaja mimba za utotoni (asilimia 56.1) ikifuatiwa na kubakwa (asilimia 46.6) na kutukanwa (asilimia 46).
- Kisiwani Pemba, asilimia 77.1 ya walioshiriki uchunguzi walitaja mimba za utotoni kuwa ni aina ya ukatili dhidi ya wanawake unoatokea mara nyingi zaidi katika jamii zao, ikifuatiwa na ndoa za utotoni (52.1), na ndoa za kulazimishwa (asilimia 39.6).
- Kisiwani Unguja, asilimia 46.6 ya walioshiriki uchunguzi walitaja uchawi (ushirikina) kuwa sababu ya Ukatili Dhidi ya Wanawake, wakionyesha kuuchukulia Ukatili Dhidi ya Wanawake kuwa ni kitu kisichoweza kudhibitiwa.
- Kisiwani Pemba, asilimia 27.1 ya walioshiriki uchunguzi waliainisha kuweka heshima ya familia kuwa sababu ya Ukatili Dhidi ya Wanawake ikiashirika uhusiano wa matatizo kati ya Ukatili Dhidi ya Wanawake na heshima ya familia.
- Majibu yaliyohusu mitazamo ya jamii kuhusu Ukatili Dhidi ya Wanawake yameonyesha mwenendo unaofanana. Wakati watu wengi walioshiriki uchunguzi wakitaja Ukatili Dhidi ya Wanawake kuwa ni hatari kwa maisha ya binadamu, asilimia 10 ya walioshiriki uchunguzi Kaskazini Unguja wanaamini kuwa wanawake ndio wanaosababisha Ukatili Dhidi ya Wanawake, na asilimia 41.7 ya washiriki Pemba walisema kwamba jamii ilifikiri kwamba Ukatili Dhidi ya Wanawake lilikuwa jambo la "kawaida".
- Kupambana na mitazamo hii kuhusu Ukatili Dhidi ya Wanawake katika visiwa vya Unguja na Pemba kutakuwa ni sehemu muhimu ya kazi za programu katika jamii hizi. Hadi hapo Ukatili Dhidi ya Wanawakeutakapotambulika kuwa ni ukiukwaji wa haki za binadamu na sio sehemu inayokubalika ya maisha ya jamii, patakuwepo na mabadiliko kidogo katika matukio ya Ukatili Dhidi ya Wanawake au kiwango cha utoaji wa taarifa.

*"Sijui njia nyingine zozote zinazofaa za kutatua masuala isipokuwa njia ile ambayo wazazi hukaa pamoja na kusuluhisha suala husika." Mshiriki wa uchunguzi, Uchunguzi wa AAITz kuhusu Ukatili Dhidi ya Wanawake.*

## Kutafuta Msaada

- Ni asilimia 22 tu ya wanawake walioshiriki uchunguzi Kaskazini Unguja na asilimia 29.8 kisiwani Pemba walioripoti kufanyiwa Ukatili Dhidi ya Wanawake ndio waliomweleza mtu mwingine kuhusu yale yaliyowatokea.
- Wanawake wengi waliotafuta msaada walifanya hivyo kwa kutafuta msaada kutoka kwa wana familia. Ni asilimia 5 tu ndio waliotoa taarifa Polisi kisiwani Unguja na asilimia 10 huko Pemba.
- Hii inaashiria kwamba wahanga wa Ukatili Dhidi ya Wanawake wanatumia njia zisizo rasmi kutafuta msaada na kwamba Ukatili Dhidi ya Wanawake mara nyingi unaonekana kuwa ni suala la jamii kuliko kosa la jinai.
- Ndoa au taratibu zisizo rasmi za kulipa fidia, ijapokuwa hazipo kisheria, mara kwa mara hutumika badala ya mfumo wa sheria za jinai Kaskazini Unguja. Utaratibu huu hufanana na ukiukwaji maradufu wa haki za mwanamke.
- Kutokuwepo kwa huduma za kuwasaidia wanawake pia kunasababisha wanawake wasijisikie wako salama kuripoti matukio ya Ukatili Dhidi ya Wanawake. Kusafiri mwendo mrefu kufuata huduma zilizopo kunaongeza ukubwa wa tatizo hili.

## Vikwazo vya Kupatikana kwa Haki

- Watu hawana imani na mfumo rasmi wa kutoa haki. Katika kuelezea ni hatua zipi Polisi watachukua katika kushughulikia ripoti ya Ukatili Dhidi ya Wanawake, asilimia 16.9 ya waliohojiwa kisiwani Unguja na asilimia 16.7 kisiwani Pemba walifikiri kwamba Polisi hawatafanya lolote au hawataipa kipaumbele ripoti hiyo.
- Mfumo wa mahakama wenye mikondo miwili na maadili ya jamii ina ushawishi mkubwa wa jinsi haki inavyotolewa na utekelezaji wa sheria kisiwani Zanzibar.
- Ucheleweshwaji wa muda mrefu, kukosekana kwa msaada wa kisheria na uwakilishwaji wa kisheria, ada za mahakama, gharama za usafiri na ufahamu mdogo wa sheria, vyote hivi vina athari katika kesi zinazoendelea katika mfumo wa mahakama.
- Wanaotiwa hatiani bado ni kwa kiwango cha chini sana kiasi kwamba hakuwezi kuzuia wahalifu au kuwashawishi waathirika kuripoti matukio ya Ukatili Dhidi ya Wanawake.
- Ujuzi mdogo wa kukusanya ushahidi, kutokuwepo kwa sera na taratibu, kukosekana kwa rasilimali na vifaa vinavyostahili bado linabaki kuwa tatizo. Asilimia 36.5 ya walioshiriki uchunguzi Kaskazini Unguja na asilimia 20.8 Pemba wameonyesha kwamba kukosekana kwa ushahidi ni sababu inayofanya kesi za Ukatili Dhidi ya Wanawake zisiripotiwe katika taasisi za sheria na zisifanikiwe kuhukumiwa ipasavyo.

*"Jamii inaogopa urasimu na ucheleweshwaji - rudi kesho, njoo tena kesho kutwa." Mshiriki wa uchunguzi, Uchunguzi wa AAITz kuhusu Ukatili Dhidi ya Wanawake*

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali ya Zanzibar imeanzisha jumuiya/vituo kadhaa muhimu vya kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake kama vile Kamati za Ukatili wa Kijinsia, Mtandao wa Polisi wanawake, Madawati ya Polisi ya kushughulikia jinsia, na hivi karibuni, kituo kinachotoa huduma nyingi mahali pamoja (Mkono kwa Mkono) katika Hospitali ya Mnazi Mmoja . Hata hivyo, kasi ya mabadiliko imekuwa taratibu na inakabiliwa na upungufu wa rasilimali. Haki, usalama, na misaada haipatikani kwa wanawake wengi walioko Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba. Uchunguzi huu unadhihirisha kwamba kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake na kuvunja "ukuta wa ukimya" unahitaji mbinu za kuzikabili/kupambana na changamoto mbili. Kwanza, maadili ya jamii na mitazamo ambayo inachukulia Ukatili Dhidi ya Wanawake kuwa ni suala la jamii na sio kosa la jinai, na kuhimiza ndoa au ulipaji wa fidia lazima zipigwe vita kupitia programu za ufahamu wa sheria na utoaji misaada kwa waathirika wa Ukatili Dhidi ya Wanawake. Pili, taasisi na huduma za sheria lazima ziimarishwe ili ziweze kutoa njia mbadala zilizo nzuri za usuluhishi usio rasmi wa makosa ya Ukatili Dhidi ya Wanawake.

# Mapendekezo

### Haki

- Kuongeza uwakilishi wa sekta ya sheria na taasisi zenye majukumu ya kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake.
- Kuanzisha kituo kikuu cha database kwa ajili ya kuweka kumbukumbu na kulinganisha taarifa za taasisi mbalimbali zinazoshughulikia wahalifu na huduma za afya na misaada. Database hii inatakiwa iwe inawezesha upekuzi kulingana na kosa, itofautishe jinsia na iweze kufikiwa na jamii nzima.
- Wakili – msaidizi wa sheria anatakiwa apatikane kwa ajili ya muathirika wa Ukatili Dhidi ya Wanawake anapokuwa kituo cha Polisi wakati wa ripoti ya awali, au kufika katika eneo la tukio la uhalifu, ili kutoa msaada na kuangalia iwapo taratibu sahihi za kipolisi zinafuatwa. Wakili – msaidizi wa sheria huyu anapaswa kuwepo ili kumsaidia mhanga wa Ukatili Dhidi ya Wanawake wakati wote wa mchakato wa mahakamani (kama vile kuhudhuria Mahakama, kuelezea taratibu, kuomba hatua zichukuliwe kumlinda muathirika).
- Kikundi kinachofuatilia utendaji katika eneo la Ukatili Dhidi ya Wanawake kitaanzishwa katika kila mkoa wa Zanzibar kikiwa na wawakilishi kutoka Serikalini, Taasisi za kusimamia sheria, Asasi Zisizokuwa za Kiserikali na huduma za afya.

### Polisi

- Kitengo maalumu cha Polisi kitaanzishwa kikiwa na jukumu la kusimamia dawati la jinsia, kushughulikia kesi za Ukatili Dhidi ya Wanawake na kujenga uwezo wa Polisi katika vituo ili waweze kuchukua hatua zinazostahili.
- Mafunzo mahususi yanayolenga wafanyakazi walioko mstari wa mbele yataanzishwa kubadili mitazamo kuhusu Ukatili Dhidi ya Wanawake, kuboresha mwitikio wa mwanzo kwa wanawake wanaotoa ripoti na ukusanyaji wa ushahidi.
- Ukatili wa Kijinsia na hasa Ukatili Dhidi ya Wanawake vinapaswa kuwa sehemu ya mafunzo ya maafisa wa Polisi. Kwa mfano, mafunzo kuhusu stadi za upelelezi zijumuishe jinsi maumivu ya Ukatili Dhidi ya Wanawake yanavyoweza kuathiri tabia za waathirika.
- Afisa wa Polisi mwanamke aweze kupatikana anapohitajika na mhanga.
- Polisi wajitahidi kuwaelekeza wanawake kwenda kwenye huduma za msaada kama vile kituo kinachotoa huduma nyingi mahali pamoja (Mkono kwa Mkono).
- Viashiria vikuu vya utendaji vionyeshe utendaji wa Afisa wa Polisi katika kesi za Ukatili Dhidi ya Wanawake.
- Polisi wapewe motisha waweze kutumia kwa vitendo stadi walizojifunza katika mafunzo ya Ukatili Dhidi ya Wanawake, kama vile kutoa tuzo za utendaji bora, motisha za fedha na kupandishwa cheo.

### Ukusanyaji wa Ushahidi

- Ukatili Dhidi ya Wanawake uwe sehemu ya mafunzo ya udaktari ili kuboresha maarifa ya ukusanyaji ushahidi na kujiamini wakati wa kutoa ushahidi mahakamani
- Kila dawati la jinsia lipatiwe Afisa Mpelelezi wa Eneo la Uhalifu ili atoe msaada wa kukusanya ushahidi. Iwapo Afisa Mpelelezi wa Eneo la Uhalifu hapatikani kuweza kufika eneo la uhalifu au kutoa huduma za msaada, itabidi daktari atumwe ili kusaidia katika kuchambua ushahidi.
- Iwapo Polisi wamefika katika eneo la uhalifu unaohusu Ukatili Dhidi ya Wanawake katika jamii, wakili – msaidizi wa sheria anapaswa pia kuwepo.
- Vituo vipewe rasilimali na vifaa vya kutosha vinavyofaa kuwezesha ukusanyaji wa ushahidi kama vile kompyuta za kuweka kumbukumbu na vyumba maalumu vilivyotengwa ili kuhakikisha faragha kwa wanawake wanaoripoti Ukatili Dhidi ya Wanawake.

**Mfumo wa Mahakama**

- Msaada wa kisheria unapaswa upatikane kwa waathirika wote wa Ukatili Dhidi ya Wanawake. Hii ijumuishe nyenzo za usafiri na gharama za kuwawezesha wanawake kusafiri kwenda kupata msaada wa kisheria na kuhudhuria vikao vya mahakama.
- Taratibu ziwekwe za kuwalinda wahanga wa Ukatili Dhidi ya Wanawake katika kesi za ubakaji na shambulio linalohusisha ngono, kama vile kutoa ushahidi kwa siri, tahadhari za kuhakikisha faragha, na viwango vya kuamua ushahidi katika kesi hizi kama vile mwongozo juu ya makubaliano ya kufanya tendo kwa hiari, hisia za kubuni na zisizobadilika zilizogubika Ukatili Dhidi ya Wanawake. Mwongozo utolewe kuelezea hatua hizi za kuwalinda waathirika.
- Mahakimu wapewe mafunzo kuhusu hisia za kubuni zinazozunguka Ukatili Dhidi ya Wanawakena pia maumivu ambayo waathirika wanaweza kuyapata wakati mahakama ikiendesha vikao vyake.
- Marekebisho yoyote ya Sheria ya Mahakama ya Kadhi (ambayo kwa sasa inafanyiwa mapitio) kama vile kuteua mawakili yanapaswa kutangazwa kila mahali.
- Mapitio na ufuatiliaji wa mara kwa mara wa taratibu za kisheria kuhakikisha zinakubaliana na vipengele vya maudhui na taratibu za sheria unapaswa kufanyika.

**Maboresho ya Sheria**

- Iainishwe kwa uhakika katika sheria kwamba ukatili unaofanyika majumbani na aina zote za Ukatili Dhidi ya Wanawake ni kosa la jina na hauko chini ya mamlaka ya Mahakama za Kadhi.
- Umri wa chini wa kufunga ndoa utamkwe katika sheria.
- Ulinzi wa kisheria unapaswa kutolewa dhidi ya kufukuzwa shule au ubaguzi dhidi ya wanawake vijana/wasichana walioolewa.
- Mali ya wanandoa ianishwe kwa uhakika katika sheria.

**Kujenga uhusiano – msaada, usalama na haki**

- Kampeni ya kuinua ufahamu izinduliwe kuelimisha jamii juu ya Ukatili Dhidi ya Wanawake, huduma zilizopo na kuwapatia wanawake ujuzi wa haki zao za kisheria. Kampeni hii ieleze kwa uhakika kabisa kwamba usuluhishi usio rasmi wa Ukatili Dhidi ya Wanawake ni kinyume cha sheria.
- Anzisha utaratibu wa wakili – msaidizi wa sheria.
- Tathmini ifanyike ya kituo kinachotoa huduma nyingi sehemu moja cha Hospitali ya Mnazi Mmoja kuhakikisha kwamba kituo kinakidhi mahitaji ya msaada wanaohitaji wanawake watu wazima. Vituo kama hivyo vianzishwe sehemu nyingine nyingi Zanzibar.
- Nyumba za hifadhi na huduma za ushauri zinapaswa kupatikana kwa wahanga wote wa Ukatili Dhidi ya Wanawake.

**Serikali**

- Mkakati wa Kisekta na Mpango Kazi wa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Maendeleo ya Watoto wa kuzuia na kushughulikia Ukatili wa Kijinsia Zanzibar unapaswa kupatiwa rasilimali za kutosha.
- Mpango kazi unaohusisha wizara mbalimbali za serikali unapaswa kutayarishwa kuhusu Ukatili Dhidi ya Wanawake, pakiwa na wafanyakazi waliopangwa katika kila Idara wenye jukumu la kufuatilia na kutoa ripoti za maendeleo.

**Mwandishi:** Sharon Smee
**Wahariri:** Dorcas Erskine na Annmarie Mavenjina
Kwa kushikiana na wafanya kazi wa AAIT na wadau wa AAITz:
Khadija Juma, Mohammed Khalid, Ismail Mgeni na Nadra Ali

Zanzibar Female Lawyers Association (ZAFELA), Jumuiya ya Wanawake Kaskazini Pemba (JUWAKAP)
na Jumuiya ya Wanawake na Maendeleo Kaskazini Unguja (JUWAMAKU)

Jarida hili limetolewa kwa msaada wa Umoja wa Ulaya. Yaliyomo katika jarida hili ni jukumu
la ActionAid International Tanzania na haihusiani kwa njia yoyote kuwekwa
katika mtazamo au maoni ya Umoja wa Ulaya.